



>>**LENGO** ni kuweka rekodi kufikia 2025>>**DED** aeleza kazi ujenzi vituo vya afya

Mikakati kabambe ya Rungwe kutokomeza vifo mama, mtoto

Na **CHARLES MGANGA**, RUNGWE

RUNGWE ni moja kati ya halmashauri saba zinazounda jiji la Mbeya lililopo ukanda wa nyanda za juu kusini mwa Tanzania.

Halmashauri zingine ni Mbeya Jiji, Chunya, Kyela, Busokelo, Mbeya DC na Mbarali.

Pamoja na kuwepo shughuli zingine, wakazi wa Rungwe wamejikita katika kilimo cha ndizi, viazi huku baadhi ya maeneo yakiwa yamelimwa chai.

Katika kutekeleza llni ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 hadi 2020, halmashauri ya Rungwe pamoja na mambo mengine, imekijita kuhakikisha afya ya mama na mtoto ni moja kati ya vipaumbele vyake ilivyotekeleza kwa kiwango kinachostahili.

Kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa miradi katika kipindi cha miaka mitano, halmashauri ya Rungwe imefanikiwa kupunguza vifo vya mama na mtoto kutoka wastani wa wajawazito 103 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2015 hadi vifo 84 mpaka kufikia mwaka jana.

Pia, vifo vya watoto 124 wenye umri chini ya miaka mitano kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2015, hadi kufikia 67 kwa kila idadi hiyo ya vizazi mpaka mwaka jana.

Taarifa ya utekelezaji wa miradi inafafanua kuwa, mafanikio hayo yanatokana na serikali kuu kuendelea kutoa rasilimali fedha na watu ili kuhakikisha mazingira ya utoaji huduma za afya yanazidi kuimarika.

Hata hivyo, halmashauri ya Rungwe imedhamiria kwamba, mpaka kufikia mwaka 2025, inataka suala la vifo vya mama na mtoto vibaki kuwa historia kwa wananchi wa eneo hilo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Rungwe, Loema Peter anasema serikali ya awamu ya tano imejitahidi katika ujenzi wa vituo vya afya na ukarabati wa miundombinu katika sekta ya

afya.

Anasema hatua hiyo, imefanya yawepo mafanikio yawepo katika utoaji huduma baada ya serikali kuu kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu.

Mkurugenzi Loema anasema serikali kuu imetoa kiasi cha sh. milioni 400 katika hospitali ya wilaya ya Rungwe ambazo zimetumika kujenga jengo kuwa la kuwahudumia akina mama na watoto.

"Jengo limekamiliwa, isipokuwa huduma za operesheni ndizo hazifanyika, lakini zingine zinaendelea kama kawaida.

"Ni jengo kubwa kwa sababu limegharimu kama sh. milioni 500 hivyo, halmashauri tulilazimika kuongeza fedha ili kuhakikisha lengo lililokusudiwa lifikiwe.

Kwa mujibu wa mkurugenzi mtendaji huyo, vituo vya afya katika maeneo tofauti, vimejengwa kupitia fedha za serikali.

Anasema halmashauri ilipokea kiasi cha sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu 13 zikiwemo nyumba za walimu, upasuaji pamoja na majengo mengine muhimu.

"Hakukuwa na huduma



MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Rungwe, Loema Peter

Kuna muda kulikuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi kwamba wanakaa foleni ndefu kwa madai watumishi wapo, wamekwenda kunywa chai au wengine wana chati.

za operesheni, ila hivi sasa zinafanyika na kuwanufaisha wananchi wa Ikuti na kati za jirani wakiwemo na watu kutoka Ileje," anasema mkurugenzi Loema.

Hata hivyo, gharama ya kazi ya ujenzi wa miundombinu ya kituo hicho cha Ikuti ilikuwa ni zaidi ya sh. milioni 700, kwa hiyo fedha nyingine zilitolewa na halmashauri, wananchi na wadau wengine wa maendeleo.

Alikitaja kituo kingine cha afyakitukilichonufaika na fedha za serikali kuu ni kile cha Masokulu ambacho pia kimepokea kiasi cha sh. milioni 500.

Anasema majengo saba yamejengwa katika kituo hicho huku halmashauri, wananchi na

wadau wakishiriki kikamilifu katika ukamilishaji wa miundombinu hiyo.

Akieleza zaidi mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya afya, mkurugenzi mtendaji huyo wa halmashauri anasema kimejengwa kituo kingine cha afya katika kata ya Isongole ambacho serikali imetoa fedha na Rais Dk. John Magufuli alichangia kiasi cha sh. milioni 30 baada ya kuwaona wananchi wa kata hiyo wamehamasika.

Anasema kuna kituo cha afya Mpuguso ambacho wananchi walianza kujenga huku fedha za mfuko wa jimbo zikisaidia na halmashauri ikichangia.

"Kituo kingine cha Masoko kiitwacho Kalebela, tulinunua kwa sababu ilikuwa mali ya mtu binafsi baada ya kushindwa.

"Tulingia mkataba kabla ya kufanya ununuzi, hivyo hivi sasa ni mali ya serikali," anaeleza Loema.

VIFAA TIBA

Anasema ili kudhibiti wizi na baadhi ya watumishi wazembe katika hospitali ya wilaya ya Rungwe, wamelazimika kufunga kamera huku changamoto kadhaa zinazojitokeza, zimekuwa zikitatuliwa.

"Katika hospitali ya wilaya, tumefunga mfumo wa CCTV ili kufuatilia kile kinachofanyika kwa siku nzima baada ya kurekodiwa.

"Kama kuna wizi au uzembe wowote unatokea, tunaangalia kupitia matukio yaliyorekodiwa.

"Kuna muda kulikuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi kwamba wanakaa foleni ndefu kwa madai watumishi wapo, wamekwenda kunywa chai au wengine wana chati.

"Sasa kupitia utaratibu huu, tunaangalia kupitia kamera tunabaini ukweli," anasema.

SEKTA YA ELIMU

Mkurugenzi Loema, anasema halmashauri imefanikiwa kukarabati shule kadhaa ikiwemo Kayuki.

Anasema shule hiyo ya wasichana yenye kidato cha tano na sita, masomo ya mchepuo wa sayansi, inayoibeba wilaya ya Rungwe, ilipokea fedha kiasi cha sh. milioni 252 kutoka serikali kuu.

"Hii inafanya vizuri sana. Ndiyo inaibeba wilaya, lakini pia kuna shule ya wavulana ya Rungwe

ambayo imepata sh. milioni 752 kutoka serikali kuu kwa ajili ya ukarabati wa majengo," anasema Loema.

MWALIMU WA BIOLOJIA

James Mwakatika ambaye ni mwalimu wa biolojia katika shule ya sekondari Kayuki anasema wanafunzi wa shule hiyo, wamekuwa wakifanya vyema kitaaluma kutokana na mazingira mazuri yaliyowekwa na serikali hasa uboreshaji wa miundombinu.

"Shule yetu tumekuwa tukifanya vyema katika taaluma siku hadi siku.

"Tunaishukuru serikali ya Rais Magufuli kwa kutoa fedha ambazo zimesaidia kuboresha miundombinu. Hapa kwetu hata nidhamu tuko vizuri.

"Haturuhusu mavazi mengine zaidi ya sare za shule. Pia, tunadhibiti hata wanafunzi kuonana na watu bila utaratibu maalumu. Wanafunzi ni mpaka likizo ndipo watakwenda kuonana na walezi. Hapa ni masomo tu," anaeleza mwalimu Mwakatika ambaye aliwahi kupata tuzo mara nne kwa ufundishaji bora somo la biolojia.

Kuhusu shule zingine zilizojengwa katika halmashari ya Rungwe, mkurugenzi mtendaji, Loema anasema zipo nne ambazo wananchi wameshiriki kikamilifu nazo ni Kalengo, Ndanto, Itagata na Ndembela I.

Anasema shule hizo ambazo zimekamiliwa na kusajiliwa, zinajendesha vizuri. Zimekamiliwa katika kipindi cha miaka mitano chini ya Rais Dk. Magufuli.

MABWENI

Loema anasema mabweni ya Suma, Masoko na Mporoto ambayo yamekamiliwa katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020, lile la Buliaga litaanza kutumika mwakani kwa sababu ukamilishwaji unaendelea.

"Haya mabweni yote yamejengwa katika kipindi hiki. Yanaendelea akutumika isipokuwa hilo la Buliaga ambalo liko eneo la umaliazaji katika sehemu kadhaa," anasema.

MADARASA

Halmashauri imeendelea kupokea fedha kutoka serikalini kwa ajili ya kuboresha madarasa.

Mkurugenzi mtendaji wa Rungwe, anasema halmashauri imepokea kiasi cha sh. bilioni 1.3 zikiwemo sh. milioni 700 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya madarasa.

KUHUSU UFAULU

Loema anasema ufaulu umezidi kuongezeka pamoja na usajili wa wanafunzi wa shule ya awali na darasa la kwanza.

Hali hiyo imefanya hata darasa la saba ufaulu nao kuongezeka kila mwaka kwani kwa hivi sasa ni asilimia 87 kutoka asilimia 58.

Anasema ufaulu wa kidato cha nne umefikia asilimia 84 huku kidato cha sita ikiwa ni asilimia 99.

"Tunafanya vizuri sana katika ufaulu, lakini haya ni matokeo chanya ya mpango wa serikali wa kutoa elimu bila malipo katika serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Magufuli," anaongeza mkurugenzi mtendaji wa halmashauri ya Rungwe.



JENGO la mama na mtoto katika Kituo cha Afya Masokulu